

HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA




TANGAZO

KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA YA ULINZI KWENYE MAJENGO YA HALMASHAURI ZABUNI NAMBA LGA/171/2021-2022/HQ/NC/01

Tarehe 23/11/2021

1. Halmashauri ya Mji wa Bunda imetenga fedha kwa ajili ya shughuli za ulinzi wa mali na majengo ya Halmashauri katika mwaka wa fedha 2021/2022.
2. Mwombaji aonyeshe uzoefu wa kazi za kutoa huduma ya ulinzi alizowahi kufanya na Serikali akionyesha anuani na mawasiliano ya sehemu alizo wahi fanya kazi hiyo.
3. Mwombaji anatakiwa kuchukua kabrasha la zabuni ofisi ya kitengo cha Manunuzi kuanzia tarehe 26/11/2021 hadi tarehe 3/12/2021
4. Mwombaji anatakiwa kuwasilisha kabrasha la zabuni iliyo jazwa kikamilifu akiambatanisha leseni ya biashara, cheti cha mlipa kodi na kibali cha kutoa huduma ya ulinzi toka mamlaka husika.
5. Mwombaji anatakiwa kufunga zabuni yake vizuri na juu ya bahasha iandikwe namba au jina la zabuni yaani "Zabuni Na.LGA/171/2021/2022/HQ/NC/01 Zabuni ya kutoa huduma ya ulinzi kwenye majengo ya Halmashauri ya Mji wa Bunda na maombi yote yawasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji wa Bunda, Kitengo cha Manunuzi.
6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 3/12/2021 saa 6.00 kamili mchana. Zabuni zitafunguliwa hadharani mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha mbele ya wawakilishi wa waombaji watakao kuwa wamehudhuria kikao cha ufunguzi. Waombaji wanaalikwa kwenye kikao cha ufunguzi
7. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo: MKURUGENZI WA HALIMASHAURI YA MJI WA BUNDA, S.L.P 219, BUNDA.

Limetolewa na:


Emmanuel J. Mkongo
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji
BUNDA